

SNAL YAPOKEA VITABU TOKA KWA PROF. AIDA C. ISINIKA



Miongoni mwa njia za kuongeza na kukuza machapisho na taarifa mbalimbali ndani ya Maktaba yoyote ile, kupokea zawadi au msaada ni mojawapo ya njia kuu mbali ya ile ya kununua.

Hivi karibuni aliyejekwa mfanyakazi na [Profesa mbobezi](#) katika Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine (SUA) Prof. Aida C. Isinika ambaye alikuwa katika Taasisi ya Elimu Endelevu ([ICE](#)) & [CoEBS](#) na ambaye amefanya kazi nyingi za ushauri katika sekta ya kilimo na maendeleo ameizawadia Maktaba ya Taifa ya Kilimo ya Sokoine (SNAL) vitabu vipatavyo 230 na hivyo kuongeza idadi ya machapisho katika maktaba hiyo.



Wakati wa makabidhiano hayo ya zawadi ya vitabu kwa Maktaba hii ya Taifa ya Kilimo, alishauri jamii kupenda kusoma na kuona maktaba kama rafiki wa karibu anayeweza kuwapa taarifa za uhakika na zenye kubadilisha jamii kimaendeleo na kifikra.

Aidha katika ushauri wake huo pia aliomba jamii za wasomi kusaidia maktaba kukua kwa kuipatia vitabu ambavyo wengi wamevifungia katika kabati zao majumbani. Alisema kwa kuvitoa vitabu

hivyo vitasomwa na watu wengi na kusaidia watu hao kupata maarifa mbalimbali kwa maendeleo yao binafsi na ya Taifa kwa ujumla.

Akipongeza na kushukuru hatua ya Prof. Isinika, Mkurugenzi wa Maktaba ya Taifa ya Kilimo ya Sokoine Prof. Camilius Sanga alipongeza hatua ya mstaaafu huyo kuizawadia Maktaba vitabu hivyo ambavyo amekuwa akivitumia kufundishia na kuandika machapisho mbalimbali kabla hajastaafu. Pia amewakaribisha wastaaafu, wasomi wengine na wadau mbalimbali kuchangia vitabu na machapisho yao ndani ya maktaba kwa faida ya Chuo chetu pamoja na wadau wake ambao ni wanafunzi, watafiti na jamii kwa ujumla.